



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



SALAMU ZA POLE

Tunduma, Tarehe 04 Disemba 2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Philemon Magesa kwa niaba ya Baraza la Madiwani, Menejimenti, Watumishi na Wananchi wote wa Mji wa Tunduma, amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyosababisha vifo vya zaidi ya watu 50 na majeruhi 85 ambayo pia yamefanya uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu katika Kijiji cha Katesh, Wilaya ya Hanang mkoani Manyara jana, Tarehe 03 Disemba 2023.

Magesa anaungana na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mhe. Ayubu Mlimba kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Queen Sendiga, Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Francis Namaumbo, Wananchi na Familia zote zilizopoteza wapendwa wao kufuatia maafa hayo.

Aidha, amesema Halmashauri ya Mji Tunduma ipo pamoja nao katika kipindi hiki kigumu na anawaomba kwa Mwenyezi Mungu waliopoteza maisha wapumzike kwa amani, anatoa pole kwa majeruhi wote na anawaomba afya njema wale walioathirika kwa kupoteza mali zao kutokana na mafuriko warejee katika hali zao za kawaida kwa haraka.


Benton J. Nollo

Mkuu Wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Mji Tunduma

*Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji, Tunduma S.L.P 73 Simu Na: 025 295 7388, Nukushi:025 295 7391, Barua
Pepe:td@tundumatc.go.tz, Tovuti:www.tundumatc.go.tz*